

Maswali

1. Jina la lango linaitwaje?
2. Mbona watu walipitia hilo lango/
3. Nani walimsimamisha Petro na Yohana?
4. Petro alimwambia nini?
5. Nini ilifanyika kwa huyo mtu?
6. Alienda wapi baadaye?
7. Petro alizungumzia jina la nani?
8. Petro aliuliza umati ufanye nini?
9. Petro alisema Yesu ako wapi?
10. Petro aliwambia ahadi kubwa gani?

Majibu

1. Lango nzuri
2. Kuomba kwa hekalu
3. Mtu kiwete
4. “Sina fedha wala dhahabu kwa jina la Yesu simama”
5. Huyo mtu alisikia nguvu kwa miguu yake na akatembea
6. Hekaluni na kushukuru Mungu.
7. Jina la Yesu
8. Watubu
9. Mbinguni
10. Kurudi kwa Yesu hapa duniani

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

47 Kuponya kwa Mlango Mzuri

Marejeo

Matendo ya Mitume 3:1—21

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba kuamini katika jina la Yesu Kristo ni vizuri

Maneno maalum

1. Mlango + Mzuri + mwombaji + tafuta usaidizi.a
2. Petro na Yakobo + kiwete + uliza.
3. Hakuna fedha + hakuna dhahabu + jina la Yesu + amka.
4. Inuliwa + simama + kimbia + furaha + miujiza.
5. Watu washangaa + umati + waambie juu ya Yesu.
6. Yesu afufuliwa + jina + maana + amini.
7. Tubu +samehe + Yesu arudi + ulimwengu mzuri.

47.1 Huko Yerusalemu kulikuwa na mlango ulioelekea kwenda kwenye Hekalu. Watu wa Yerusalemu walidhani kwamba Hekalu ni jengo nzuri. Kwa hivyo huo mlango ulikuwa wa maana na uliitwa mlango nzuri. Nje ya mlango kulikuwa na waombaji waliokuwa wakiomba waendao Hekaluni.

47.2 Siku moja baada ya Yesu kwenda Mbinguni, Petro na Yohana walikuwa wakienda Hekaluni kuomba. Walisimamishwa na mtu kiwete. Alikuwa kiwete tangu kuzaliwa kwake, kwa hivyo hajawahi kutembea. Alikaa langoni akiomba, siku hiyo aliomba Petro na Yohana wamsaidie.



47.3 Petro alimkazia macho. Akanena maneno ya kushangaza, “Sina Fedha wala dhahabu lakini nina kizuri zaidi cha kukupa.” Akasema, “Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti simama utembea.”

47.4 Petro alinyosha mkono wake. Yule mtu akamshika na akamwamrisha kusimama. Punde tu, akapata nguvu miguuni mwake. Ilikuwa mara yake ya kwanza kusimama. Alitembea, akuruka na kukimbia. Ilikuwa siku yake kubwa na ya furaha katika maisha yake, alikimbia hapa na pale akiruka kwa ajili ya zawadi kubwa aliyopewa na Petro na Yohana.

Baadaye alikumbuka kwamba lazima ashukuru Mungu kwa zawadi ya kuponywa. Mungu aliwezesha muujiza ukafanyika. Yule mtu alifwata Petro na Yohana wakaenda wote hekaluni.



47.5 Muda si muda kila mtu alisikia juu ya muujiza, na wakaanza kukusanyika. Walishangaa walipoona huyo mtu anatembea na kuruka. Walijua Petro na Yohana walifanya hayo maajabu. Petro aliwambia kwamba amepona kwa jina la Yesu. Kwa haraka Petro alianza kuwazungumzia. Alitumia uponyaji wa huyo mtu kuambia watu juu ya Yesu.

47.6 Aliwambia Mungu alimtuma mwanawe kwa watu wa Israeli. Watu wa Yerusalemu walipasa sauti zao na kusema asulubishwe, hawakujua alikuwa mwokozi wao. Mungu alikuwa amemfufua. Hii ilifanya jina la Yesu liwe na umuhimu. Kuamini katika jina la Yesu ndio ilimponya kiwete.

47.7 Petro waliwauliza wote watubu. Ingawaje walimsulubisha Yesu, lakini inawezekana wamrudie Mungu kupitia kwa yesu, dhambi zao zaweza kusamehewa.

Petro aliwambia kwamba Yesu ako mbinguni anangojea Mungu amtume hapa duniani. Manabii walisema atafanya kila kitu kizuri kama vile kulikuwa kwa bustani ya Edeni Huyo mtu kiwete aliwezeshwa kutembea. Yesu atakaporudi atafanya kila kitu kizuri tena.